MTAZAMO

BAKARI KIMWANGA

Marufuku ya mkaa na kisa cha kitatange

HIVI karibuni Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Huduma za Misitu Tanzania (TFS), ilitangaza kupiga marufuku usafirishaji wa mazao ya misitu, ikiwamo mkaa, ambapo mfanyabiashara anayefanya biashara hiyo atapaswa kuwa na vigezo ambavyo Serikali inavihitaji, tofauti na hapo sheria itachukua mkondo wake.

Zuio hilo linakwenda sambamba na kupiga marufuku usafirishaji wa magogo ya miti kwenda nje ya nchi, magari kubeba mbao yakiwa yamefunikwa, pikipiki na baiskeli kubeba mkaa kwenda sehemu moja hadi nyingine mijini na vijijini.

Marufuku hiyo ilitangazwa na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Profesa Dos Santos Silayo, akisema uamuzi huo ni moja ya mikakati ya kukusanya maduhuli stahiki ya rasilimali za misitu na kuwabana wakwepa ushuru.

Nabaki kuwa mtazamaji, ikiwa leo ni Siku ya Mazingira Duniani, huku nikishuhudia namna Serikali inavyohaha na marufuku yake kwa kuwa na kauli kinzani, ikiwamo kujishangaa na hali hiyo.

Tunashuhudia ipo misitu ambayo inaweza kuwa ya asili au ya kupandwa na binadamu (isiyo ya asili). Misitu ya asili ni misitu ambayo huota yenyewe bila kupandwa na mwanadamu. Kwa mfano, msitu wa Udzungwa (Mkoa wa Morogoro).

Misitu isiyo ya asili ni misitu ambayo hupandwa na mwanadamu. Ndiyo tofauti kati ya misitu ya asili na isiyo ya asili.

Mara nyingi wanyama mbalimbali, wakubwa kwa wadogo, huishi na hutegemea uoto huo wa asili kwa kuwatimizia mahitaji yao kwa malazi na chakula.

Hata hivyo, maisha ya binadamu hutegemea mazingira yake yanayomzunguka katika kujikimu, kwani kupitia misitu mvua hunyesha na hivyo kusababisha ustawi na ongezeko la chakula.

Ni kwamba asilimia kubwa ya watu hutegemea kilimo ili kujipatia mahitaji yao ya kila siku, hasa katika nchi za Afrika, ambazo ziko nyuma sana katika nyanja za utumiaji wa teknolojia za kisasa, kama utumiaji wa zana za kilimo.

Hivyo katika kutimiza upatikanaji wa chakula kwa wingi, ni lazima misitu ilindwe kwa nguvu zote katika ukuaji na ustawi wa jamii.

Tunatakiwa tutunze misitu kwa ajili ya manufaa yetu wenyewe na vizazi vingine, kwa sababu misitu inatusaidia kwa utalii na tunaweza kupata mvua.

Zipo faida nyingi zitokanazo na misitu, ikiwamo kusaidia mfumo wa mvua, kutumia kama makazi ya wanyama, chanzo cha mapato ya nchi, hutupatia dawa na chakula na mbao kwa ajili ya ujenzi.

Ni wazi maeneo mengi ya misitu, hasa ya asili, yapo vijijini ambako kwa kiasi kikubwa walinzi wake ni wananchi wenyewe, ambao ndio wanatakiwa kuilinda kwa kila hali.

Hata hivyo, hatua ya Serikali kuweka zuio ya marufuku ya kusafirisha mitaa kutoka wilaya moja kwenda nyingine huenda kuna lengo zuri, lakini bado kuna ukakasi katika hili, kwani ni wazi kwa tafsiri nyepesi sasa tunatakiwa kutumia nishati ya gesi.

Wakati uamuzi huu ukichukuliwa, bado maeneo, hasa ya miji mikubwa kama Dar es Salaam, hakuna msitu wa aina yoyote.

Ni wazi hatua hii sasa huenda ikachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu mkubwa wa mazingira, ikiwamo uharamia kupitia miti kwa kukatwa na watu kuchoma mkaa ambao huenda ukasafirishwa usiku wa manane.

Katika kuendelea au kusimamia marufuku ya matumizi ya mkaa kama njia ya kulinda rasilimali miti, bado tuna changamoto kadhaa ambazo Serikali inatakiwa kutafakari kwa kina, badala ya kukimbilia kupiga marufuku matumizi ya mkaa.

Nishati ya mkaa imekuwa ikitumiwa na wananchi wengi wa mijini na vijijini, lakini unahitajika usimamizi mzuri, ikiwamo kuvipa nguvu vijiji ili viwezi kunufaika nayo.

Ikiwa vijiji vitapewa nguvu badala ya kutegemewa TFS ambao wamekuwa wakikusanya mapato na kuviacha vijiji vikibaki kuwa waangaliaji, itasaidia misingi ya utawala bora na uwazi kwenye misitu.

Kwa mujibu wa takwimu, asilimia 94 za kaya zote takriban milioni tisa nchini zinatumia mkaa kama nishani kuu, huku maeneo ya mijini pekee ikiwa na asilimia 38 za watumia mkaa.

Ni wazi kwa mujibu wa mamlaka, Taifa linahitaji miti mita za ujazo 62.3, huku uwezo ukiwa ni mita za ujazo 42.8, hivyo uharibifu wa misitu unafika hekta 372,000 kwa mwaka, sawa na asilimia 1.1 ya eneo lote lenye miti.

Kwa takwimu hizo, miti na misitu nchini imekuwa ikipungua kwa kiasi kikubwa na kusababisha uhitaji wa hekta mpya 185,000 za misitu inayotakiwa kupandwa maeneo mbalimbali ya nchi.

Ama kweli uzuiaji huu wa mkaa kwa matamko tata ninaufananisha na kisa cha kitatange kilichotanga na hatimaye kimeingia demani.

> Ni wazi hatua hii sasa huenda ikachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu mkubwa wa mazingira, ikiwamo uharamia kupitia miti kwa kukatwa na watu kuchoma mkaa ambao huenda ukasafirishwa usiku wa manane.

MWANDISHI WETU

Rasilimali misitu zinufaishe jamii yetu

> Lengo la kampeni hiyo ni kuleta mageuzi chanya ya utawala bora katika misitu na kupunguza uvunaji haramu wa misitu pamoja na kuongeza faida zitokanazo na misitu kwa jamii ziishizo kando ya misitu.

UHIFADHI wa mazingira umezidi kuwa kama wimbo unaoimbwa kila kukicha, lakini bado hali imekuwa mbaya.

Pamoja na hali hiyo, lakini kinachoshangaza ni kuwa, licha ya kuhamasisha na uwepo wa kampeni mbalimbali kupitia marafiki wa maendeleo kuhusu kuhifadhi mazingira, mataifa mengi, ikiwamo Tanzania, bado yanakabiliwa na matatizo mengi yanayotokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Tunaadhimisha Siku ya Mazingira Duniani, lakini bado kuna changamoto lukuki, hasa katika utawala Bora wa Misitu kupitia rasilimali za misitu ambazo zimekuwa msaada mkubwa katika kuendesha maisha ya Watanzania wengi.

Kwa sasa hali ya uvunaji uliozidi kiwango, matumizi mabaya na utawala dhaifu umekwaza uwezo wake wa kuchangia lengo kuu la maendeleo la taifa.

Taarifa ya mwaka 2007, iliyoandaliwa na TRAFFIC, imeonyesha dhahiri mapungufu makubwa ya kijamii, kimazingira na kiuchumi katika biashara ya magogo Tanzania.

Kampeni ya Mama Misitu, kupitia washirika wake, wameainisha vyanzo vya mapungufu katika utawala bora wa misitu ambayo kampeni hii inakusudia kuyaweka wazi:

Wanajamii hawana ufahamu wa kutosha kuhusiana na haki zao katika misitu na ardhi ya misitu;

Sera na Sheria za misitu hazitekelezwi, lakini bado utawala wa sheria ya ardhi haufahamiki.

Usimamizi huria katika wa sekta ya biashara ya mazao ya misitu na kuwapo kwa udanganyifu na vitendo haramu katika mlolongo mzima wa biashara ya magogo.

Kampeni ya Mama Misitu ilizinduliwa kwa mara ya kwanza 2008 na Kikundi Kazi cha Misitu Tanzania- TFWG, ambapo iliongozwa na Jumuiko la Maliasili Tanzania-TNRF na kuzinduliwa tena rasmi kwa kipindi cha miaka mitano, ikiwa ni kuendeleza uelewa na kupanua wigo wa kampeni kutokana na uzoefu na yaliyojiri katika kipindi cha majaribio cha mradi.

Lengo la kampeni hiyo ni kuleta mageuzi chanya ya utawala bora katika misitu na kupunguza uvunaji haramu wa misitu pamoja na kuongeza faida zitokanazo na misitu kwa jamii ziishizo kando ya misitu.

Licha ya hali hiyo, nchi yetu bado iko njiapanda pamoja na kuwa na nchi nzuri yenye bioanuai za wanyama na mimea ambazo haziwezi kufananishwa na nchi nyingine yoyote. Takriban asilimia 40 ya eneo lote la nchi limehifadhiwa kwa ajili ya misitu na wanyamapori.

Hata hivyo, uharibifu wa misitu unafanyika kwa kasi ya kutisha. Takriban ekari milioni moja za misitu zinateketezwa kwa mwaka na karibu mabonde na mifumo yote ya mito mikuu hapa nchini inaanzia kwenye misitu ambayo sasa tunaiharibu kwa kasi ya kutisha.

Kuna mambo kadhaa yanayochangia kasi hii kubwa ya uteketezaji wa misitu hapa nchini, ikiwamo ufyekaji wa maeneo kwa ajili ya kilimo, mifugo, uchomaji wa mkaa na biashara ya kuni.

Hakuna shaka kwamba mahitaji ya mkaa na kuni yanazidi uwezo wa misitu yetu ya asili kukidhi mahitaji hayo. Mahitaji haya yataendelea kuongezeka kwa kasi kwa miaka inayokuja kutokana na ukuaji wa miji na ongezeko la idadi ya watu, kwani inaaminika kwamba ongezeko la asilimia moja ya ukuaji wa miji linasababisha ongezeko la asilimia 14 la matumizi ya mkaa.

Ikizingatiwa kwamba Tanzania ni moja ya nchi zinazoongoza duniani kwa kasi ya ukuaji wa miji, kiasi kwamba ifikapo mwaka 2027 zaidi ya nusu ya Watanzania watakuwa wanaishi mijini, mahitaji na matumizi ya mkaa yatakuwa maradufu kuliko ilivyo sasa.